

Imetolewa tarehe: 06 Mei, 2010

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHA NA KUDHIBITI MATUMIZI YA SINDANO ZA KAWAIDA (STANDARD DISPOSABLE SYRINGES) NA KUIMARISHA MATUMIZI YA SINDANO ZINAZOJIHARIBU BAADA YA MATUMIZI (AUTODISABLE SYRINGES)

Katika kutekeleza sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu sindano salama na udhibiti wa uchafu unaotokana na huduma za afya kwa lengo la kulinda usalama wa wagonjwa na kutumia teknolojia mpya, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) iliandaa mkutano wa wadau mnamo tarehe 1 Septemba 2009, ambapo mapendekezo ya kusitisha na kudhibiti matumizi ya sindano za kawaida na kuimarisha matumizi ya sindano zinazojiharibu zenyewe baada ya matumizi yalijadiliwa na kukubaliwa na wadau.

Sindano zinazojiharibu zenyewe ni aina ya sindano ambazo haziwezi kutumika zaidi ya mara moja kwa vile zinajiharibu zenyewe baada ya matumizi. Pia kuna aina nyingine za sindano ambazo haziwezi kurudiwa kutumiwa baada ya kuharibiwa kwa hiari na mtumiaji.

Kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa baina ya Mamlaka na Wadau mnamo mwezi Septemba 2009, TFDA inapenda kuutangazia umma kwamba kuanzia tarehe **1 Mei 2010** haitatoa vibali vya kuingiza sindano za kawaida na sindano zinazoharibiwa kwa hiari za ujazo wa mililita 10 na chini yake isipokuwa kama zitatumika kwa ajili ya matumizi maalum kama vile ulishaji wa chakula kwa njia ya pua na kutolea damu. Mwongozo wa uingizaji wa sindano za kawaida kwa ajili ya matumizi maalum utatolewa na TFDA.

Sindano za kawaida za ujazo wa zaidi ya mililita 10 zitaendelea kutumika bila masharti mpaka hapo taarifa nyingine itakapotolewa.

Ili kuhakikisha kwamba kipindi cha mpito pamoja na mabadiliko haya ya kisera yanafanikiwa, ilikubaliwa kwamba muda wa miezi tisa utolewe ili makampuni ambayo yataathiriwa na mabadiliko haya yaweze kumalizia sindano zilizopo na kuanza kutumia sindano zinazojiharibu zenyewe. Muda wa miezi tisa umepangwa kuanza tarehe 1 Mei 2010 hadi tarehe 31 Januari 2011.

Vibali vya uingizaji wa sindano zinazojiharibu zenyewe vitatolewa tu endapo sindano husika zitakuwa zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kusajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa.

Waingizaji wote wa sindano wanashauriwa kuwasiliana na TFDA ili kupata mwongozo wa ziada kuhusu viwango vya ubora vinavyokubalika vya sindano zinazojiharibu zenyewe sanjari na taarifa nyingine zinazohusiana na taarifa hii.

Limetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Barabara ya Mandela, Mabibo-External,
S.L.P 77150, Dar es Salaam.
Simu: +255 222 450512/450751/452108
Nukushi: +255 222 450793
Barua Pepe: info@tfda.or.tz; Tovuti: www.tfda.or.tz**

Ofisi za Kanda :

TFDA – Kanda ya Ziwa,
Mtaa wa Nkurumah,
S.L.P. 543,

Mwanza.

Simu: +255 28 2500733
Nukushi: +255 28 2541484
Barua Pepe: mwanza@tfda.or.tz

- TFDA – Nyanda za Juu Kusini,
Jengo la Mkoa la Mifugo,
S.L.P. 6171,

Mbeya.

Simu: +255 25 2504425
Nukushi: +255 25 2504425
Barua Pepe: mbeya@tfda.or.tz

- TFDA – Kanda ya Kaskazini,
Eneo la Sakina,
S.L.P. 16609,

Arusha.

Simu: +255 27 2547097
Nukushi: +255 27 2547098
Barua Pepe: arusha@tfda.or.tz

- TFDA – Kanda ya Mashariki,
Jengo la Makao Makuu ya TFDA,
Barabara ya Mandela, Mabibo-External,
S.L.P. 77150,

Dar es Salaam.

Simu: +255 22 2450512/2450751/
2452108
Nukushi: +255 22 2450793
Barua Pepe: info@tfda.ot.tz